

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

### WIZARA YA AFYA



#### TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU UGONJWA USIOFAHAMIIKA MKOA WA LINDI

**13/7/2022, Dodoma**

**Ndugu Wananchi**, Tarehe 7/7/2022, Wizara ya Afya ilipokea taarifa toka kwa Mganga Mkuu Mkoa wa Lindi kuwa katika Halmashauri ya Ruangwa kumekuwepo na Ugonjwa usio wa kawaida kutoka Kituo cha Afya Mbkenyera, ambapo Ndani ya siku 3 (tarehe 5 na 7 July 2022) walipokea Wagonjwa 2 katika kituo hicho wakiwa na dalili za homa, kuvuja damu (hususan puan), kichwa kuuma na mwili kuchoka sana.

Wizara iliunda timu ya wataalam kutoka idara ya Magonjwa ya dharura na Majanga, Epidemiolojia, Mkemia Mkuu wa Serikali, Taasisi ya Utafiti (NIMR), Chuo kikuu cha Sayansi ya Tiba Muhimbili na Hospitali ya Taifa Muhimbili, waliungana na timu ya Mkoa ikihusisha pia Idara ya Mifungo.

Hadi kufikia tarehe 12 Julai kulikuwa na jumla ya **wagonjwa 13, kati yao, 3 wamefariki**. **Wagonjwa wawili (2) waliokuwa wametengwa katika kituo cha Afya Mbkenyera**, wamepona na kuruhisiwa kurudi majumbani mwao. **Wagonjwa wengine 5 wamejitenga katika makazi yao ya muda kwenye kitongoji cha Naungo, Kata ya Nanjilinji Wilayani Kilwa**. **Mgonjwa mmoja ambaye amepona, anaendelea kufanya shughuli zake kijijini Mbkenyera**. Vile vile watu walitangamana na wagonjwa hao (contacts) wamekuwa wakifuatiliwa afya zao kila siku na hadi sasa hakuna

aliyeonesha dalili zozote zinazofanana na za wagonjwa hao. **Timu inaendelea na ufuatiliaji**


**Ndugu Wananchi**, Sampuli za awali zilizopimwa katika maabara ya Taifa zimeonesha majibu **hasi (negative)** kwa ugonjwa wa **Ebola, Marburg na UVIKO-19**. Tunaendelea kufanya uchunguzi zaidi wa kiepidemiolojia na kitabibu pia tunasubiri matokeo ya vipimo zaidi vya maabara ya magonjwa ya Binadamu, Wanyama na Mkemia Mkuu wa Serikali. Pia tunaendelea kufanya yafuatayo;

- a. Kuendelea kutafuta watu wengine wenye dalili kama hizi ili kutambua mapema na kuwatenga ili kuzuia ugonjwa usisambae
- b. Kuwatambua watu wote waliotangamana (Contacts) na wagonjwa/wahisiwa/marehemu na kuwafuatilia kwa siku 21
- c. Kutoa matibabu kwa wagonjwa waliobainika kuwa na dalili pia kuwashauri wajitenge wakati wakisubiria majibu ya vipimo vya maabara
- d. Kutoa elimu kwa jamii kwa kutumia vyombo mabalimbali vya habari
- e. Yamefanyika Maandalizi ya dawa, vifaa tiba na vifaa vya kujikinga na maambukizi kwa ajili ya kuwashudumia waathirika endapo watajitokeza tena

Taarifa ikikamilika Wizara itatoa taarifa kwa umma.

**Ndugu Wananchi**, Pamoja na hayo, Wizara inatoa wito kwa wananchi kuwa watulivu wakati ikiendelea kulifanyika kazi suala hili. Aidha Wananchi waendelee kutumia Vituo vya kutolea huduma za afya pale wanapojisikia kuumwa.

Imetolewa na,



Dkt. Aifello W. Sichalwe  
**Mganga Mkuu wa Serikali**